# UJUMBE WA JENERALI WA MWAKA MPYA 2023 - CHAPISHA TOLEO

**Mara moja Basi**

Wapendwa Marafiki,

Mwaka Mpya huwa mara zote unabeba uwezo mkubwa na wengi wetu tunatumia muda fulani tukifikiria kuhusu mandhari iliyoko mbele yetu. Tunatafakari maazimio ya Mwaka Mpya, tunazingatia 'kuanza tena' – kuwa na mwanzo mpya au kuwa na ukurasa msafi. Nyakati nyingine, kuna mambo tunayotaka tuyaache nyuma na kitu kinaibuka ndani yetu kikipendekeza kwamba jitihada makini za kibinadamu za kulenga upya zitaleta tofauti. Kila mwaka sauti huja: 'safisha tendo lako'; 'unaweza kufanya vizuri zaidi'; 'kamata'; 'usiwe huna mpangilio'; 'zingatia mambo sahihi'. Sio rahisi kila mara kuanza vizuri!

Kama nilivyokuwa nafikiria kuhusu uwezo wote huo na kujaribu kwa bidii, nakumbushwa kuhusu simulizi za Agano la Kale za watu ambao kila mara walifanya jitihada kubwa za kupata mahusiano sahihi na Mungu. Kama wao, na sisi tunajitahidi sana, na tunafanya mazoezi ya dhehebu letu, tukitarajia yote yatakuwa sawa.

Kama haya yanakudhirisha wewe na hivyo ndivyo unavyojisikia unapoukaribisha mwaka wa 2023, nina habari njema ambayo imeunganika na jinsi tutakavyouanza Mwaka huu Mpya na namna gani tutayafanya mambo yawe sawa.

Nataka nikutambulishe kwake **'Mungu wa mara moja na kwa wote'** (Warumi 6:10:'Maana kwa kule kufa kwake, aliifia dhambi mara moja tu; lakini kwa kule kuishi kwake, amwishia Mungu.'). Kwa wengine inaweza kuwa mtazamo mpya lakini, una historia. Utoaji wa Mungu kwetu ulianza na Agano Jipya likianza na msalaba. Huu ni mtazamo wa yale ambayo Mungu ametutendea na sio kwasababu ya jitihada na bidii yetu. Ni mwanzo mpya uliozaliwa katika kujisalimisha kikamilifu kwa mtu binafsi.

Kwa hiyo ingia katika Mwaka huu Mpya kwa kujiamini, sio kujiamini kule kunakotokana na jitihada zako za kibinadamu bali kujiamini kunakotokana na kutembea na 'Mungu wa mara moja na kwa wote' anayesema, 'neema yangu yakutosha'.

Waebrania 9:28 inasema: 'Kadhalika Kristo naye, akiisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi.' Hiyo ni pamoja na sisi. Yohana 1:29 inasema:'…Tazama mwana kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!' Hizo ni dhambi zangu na zako.

Katika ukweli kwamba Kristo alikufa mara moja kwa wote, kuna ukweli vile vile kwamba anaishi, na kwasababu anaishi sisi tunaweza kuishi vile vile. Kutembea na Mungu kila siku, hutufanya tukabiliane na yale ya muda na ya kiroho katika njia ambayo hata lije lipi, ukweli wa tendo la Mungu kwa niaba yetu linabakia kuwa mwamba imara. Hiyo ina maana kwamba, lije lolote – kama uchumi ukishindikana, kama afya italeta changamoto, kama mipango yetu itavurugwa, na hata kama tunaloogopa sana litatokea – **sisi tuko salama mikononi mwake, tukitambua kwa hakika msaada wake.**

OFFICE OF THE GENERAL
INTERNATIONAL HEADQUARTERS

Katika eneo la kujitoa pana ning'inia bango, linalosomeka: 'Mungu yuko pamoja nasi naye ni mwaminifu'. Kwa msingi huo tunaweza kuingia katika kila siku ya mwaka mpya kama 'zaidi ya washindi' (Warumi 8:37), na katika ufahamu kwamba Kristo 'ameushinda ulimwengu' (Yohana 16:33), kwasababu neema yake inatutosha naye ni mwaminifu.

Warumi 5:8 inafunika hili: 'Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.' Imetendeka! Mara moja na kwa wote….na hilo hubadilisha yote.

Mungu akubariki kwa wingi mwaka mzima wa 2023.

Brian Peddle
Jenerali